

MAELEZO YA MSINGI KUHUSU MAGONJWA NA WADUDU WA MIKOROSHO

1. MAGONJWA

1.1 Anthraknose

Ugonjwa huu hushambulia sehemu change za mkorosho na husababisha hasara kubwa kama ukishambulia maua, kwani maua huwa meusi na kufa. Maua yanapokufa mkorosho hawezi kuzaa. Ugonjwa huu huendelea kuanzia kwenye vikonyo vya matawi na kuuwa tawi zima. Vimelea vya ugonjwa huu huzaliana sana kwenye hali ya unyevu na joto.



Nini cha Kufanya

- Pruni/kata matawi yote yaliyoshambuliwa na uyaondoe shambani
- Japokua dawa za kuuwa vimelea vya magonjwa kweye mikorosho hazitumiki sana hapa Afrika Mashariki, ugonjwa huu huweza kuthubitiwa kwa kupulizia dawa iitwayo Bordeaux mix ambayo imeruhusiwa kwenye uzalishaji endelevu kama ikitumika ipasavyo. Inashauriwa kuuliza kwa mamlaka inayothibiti uzalishaji endelevu kabla ya kutumia.

1.2 Ubwiri Unga/Ukungu (Powdery Mildew)

Ugonjwa huu ni tatizo kubwa sana nyanda pwani na meneo ya Mtwara. Majani na maua yaliyoshambuliwa huwa na ukungu mweupe. Kama usipozuiwa mapema korosho hushindwa kuzaa.



Nini cha Kufanya

Japokuwa wakulima wengi hawanyuzii mikorosho dawa, inashauriwa kutumia dawa iitwayo **Sulfur** kadiri ya maelezo yaliyoandikwa. Dawa hii isinyunyuziwe shambani ndani ya siku 20-30 baada ya kutumia dawa nyingine na pia kusiwe na joto kali. Halijoto inatakiwa kuwa chini ya nyuzijoto 26°C.



2. WADUDU WANAOSHAMBULIA KOROSHO

2.1 Mbu wa Korosho

Wadudu hawa ndio wadudu hatari sana wa korosho, ni walaini na waliochongoka, wenye antenna na miguu mirefu. Majike huwa na rangi nyekundu na madume huwa na rangi ya vumbi inayokaribia nyekundu. Huanza kushambulia mimea wakiwa kwenye hatua ya ukuaji kabla ya kufikia mdudu kamili.

Hushambulia majani machanga, matawi yanayochipua na kutoa maua. Pia hushambulia matunda yanayokua. Majani yaliyoshambuliwa huharibika na kuonekana na michoromichoro kwenye vishipajani. Majani huweza kudondoka na kuonekana kama yameshambuliwa na wadudu wanaotafuna majani. Kama wadudu hawa wakiwa wengi sana korosho huonekana kama imeunguzwa na moto.

Mbu hawa wakishambulia matunda yanayokua husababisha alama zilizozama zenye rangi ya vumbi kwenye kokwa la korosho.

Mikorosho iliyoshambuliwa na ugonjwa huu hukua kwa shida na huwa na uwezo mdogo wa kutoa matunda.

Nini cha kufanya

- Chunguza mazao mara kwa mara, kwani mbu hawa hutokea ghafla hasa kipindi cha mvua ama kukiwa na maji ya kutosha wakati mbao korosho huchipua sana.
- Hifadhi wadudu marafiki wa mkulima. Mfano chungu wanaosuka nyuzinyuzi kwenye mkorosho huzuiya mdudu huyu na wengine wanaofanana nae. Maji moto ambao hupatikana sana kwenye miembe pia hufaa kukinga dhidi ya nzi wa korosho.
- Usichanganye korosho na mazao yanayokaliwa na mbu wa korosho pamoja shambani. Mazao hayo ni kama pamba, chai, viazi vitamu, mapera na maembe.



2.2 Mbu wa mnazi

Wana rangi ya kahawia nyekundu wakiwa wakubwa. Hunyonya majani na kusababisha alama zilizoanza kuoza. Hunyonya matunda yanayokua na kuacha alama. Madhara haya husababisha kupungua kwa thamani ya korosho sokoni au pindi inapouzwa.

Nini cha kufanya

- Hifadhi wadudu marafiki wa mkulima. Mfano chungu wanaosuka nyuzinyuzi kwenye mkorosho huzuiya mdudu huyu na wengine wanaofanana nae.



Wadudu wengineo

Mealy bug



Kifa uwongo

